



BIASHARA KWA MTANDAO

PART 1

INTRODUCTION TO

JINSI YA

KUAGIZA BIDHAA KWA USALAMA

VYA

KUZINGATIA KABLA YA KUAGIZA

JINSI YA

KULIPIA NA KUPOKEA MIZIGO

JINSI YA

KUTO POTEZA MZIGO NA KUUPATA KWA HARAKA

NA MENGINE MENGI.....

WRITTEN BY:

M*kwanzania*.COM

CHAPTER 1 : Kupata kadi na account za kufanya manunuzi mtandaoni.....

-kadi ninazotumia kufanya malipo na kuagiza bidhaa kwenye mtandao.....

-nyongeza verified account ya paypal ndani ya nusu saa).....

CHAPTER 2: Kutafuta bidhaa (pamoja na tovuti ambayo tutakua tunaitumia sana).....

Chapter 3 : Kutengeneza brand.....

Chapter 4: Vya kuzingatia kabla ya kuagiza bidhaa yoyote kutoka mtandaoni.....

Chapter 5: Jinsi ya kutafuta muuzaji anaeaminika

Chapter 6: Shipping option zote na maelezo yake.....

Chapter 7: Jinsi ya kutrack mizigo yako vizuri.....

Conclusion.....

Introduction to kuagiza bidhaa kutoka nje kwa ambae hajawahi hata mara moja.

Kwenye hii PDF itakua inaelezea na kufundisha kutoka mwanzo kabisa, yaani tunachukulia kuwa mtu ambae hajui kabisa wapi pa kuanzia, hana idea yoyote, hajawahi hata kufanya manunuzi online hata mara moja, hapo ndo tunapoanzia so kama wewe una ujuzi kidogo unaweza uka ruka baadhi ya chapter. au ukaenda kucheki advanced course [kwenye link hii japa](#)



CHAPTER 1 : Kupata kadi za kufanya manunuzi mtandaoni



-Kadi za ninazotumili kufanya malipo kwenye mtandao

Ili kufanya manunuzi online, unachohitaji ni kadi yako ya account ya benki iliyunganishwa na visa ama mastercard, au kadi ya visa au mastercard inayokua issued na benki. Hivi ni vitu viwili tofauti. Inaweza ikachanganya baadhi ila ngoja nizielezee kidogo hapa chini na kwanini napenda kadi ya pili hiyo.

i) Kadi ya account ya benki yenye uwezo wa mastercard au visa

-Hii ni account ya kawaida kama tunazozitumia kila siku za benki, ila zina onganishwa na huduma ya visa/mastercard.

Makato yake ni madogo sana huu ndo uzuri wa account za benki, ila account za benki zina restrictions nyingi, mfano account nyingi za benki nilizo experience zina limit ya mara ngapi unaweza kufanya manunuzi mtandaoni.

Kwa mfano kadi ya CRDB ilikua ni ukifanya manunuzi mara tatu ndani ya nusu saa mara ya nne kadi inakataa, hela inakatwa lakini malipo hayaendi, so inabidi kufuatilia benki mda mrefu hela irudi karibia wiki nzima mda mwingine.

So mfano wa hapa ambao ntashauri kadi ya kutumia ni benki ya **CRDB**.



Kama tiyari una account CRDB, unachotakiwa kufanya ni kwenda kwenye tawi lolote na kuomba wa ruhusu kadi yako iweze fanya malipo online. Utajaza form moja, na kadi yako itakua na uwezo wa kufanya malipo mtandaoni.

Kuna benki nyingine nyingi ambazo wana offer huduma za Kufanya malipo online kupitia kadi zao, ila CRDB ndio nitayo recommend kwa kuwa nimeitumia na haina matatizo mengi when it comes to kufanya malipo mtandaoni, wengine unaweza kujaribu KBC au NBC. Kama tiyari una bank account na unataka tumia hiyo, unaweza enda uliza kwenye tawi lako lililo karibu kama wanaruhusu kufanya malipo mtandaoni kama hawafanyi ndio utafute benki nyingine.

Cha kuzingatia: Huwa sipendi tumia account personal za benki kufanya manunuzi online, ni bora ukafungue account nyingine pembeni ndiyo uwe unafanya nayo manunuzi kwenye mtandao.

ii) Visa /Mastercard inayo kuwa issued na benki

Hizi ndio card ninazo zi prefer mimi, hauhitaji account ya benki kupata kadi kama hizi, zinakuwa issued na baadhi ya benki na unaweza pata kadi kama hizi ndani ya nusu saa tu.

Makato yake ni ya juu kidogo kuliko account za benki nilizozielezea hapo juu, sanasana inaongezeka kati ya sh 500 – sh 2,000 kwa kila transaction/manunuzi unayofanya (inategemea na kiasi unacholipia).

Except for that, hizi kadi ndio the best kwa ajili ya manunuzi ya mtandaoni, hazina restrictions nyingi na ni rahisi ku manage account yako. Kadi ninayotumia mimi na ambayo ipo reliable ni hii hapa. (mfano huu)



Kadi kutoka UBA

Bank kama **UBA** unaweza kupata kadi za visa bila hata kuwa na account, unaweza kupata kadi yenye uwezo wa kufanya malipo online ukienda tu na kujaza information zako. Kadi zinakuwa zipo tiyari, unaweza kuweka hela kwenye kadi hizi kwa tigopesa/mpesa au kwenda kwenye tawi la karibu.

Uzuri wake hapa ni kuwa hawana uzungushaji sana kama kuna tatizo kwenye malipo, hela zako zinarudi ndani ya lisaa kama kuna chochote kimetokea, haijawahi kuwa na tatizo toka nianze kutumia.

So kwa ataetaka kufahamu kadi ninayotumia kipindi nafanya manunuzi mtandaoni bila tatizo lolote, ni visa card kutoka benki ya UBA.

Kwa dar-es-salaam matawi ya UBA nnayo yafahamu yapo posta mpya na kariakoo. Ukienda ulizia kupata kadi ya visa. Kwa nje ya dar-es-salaam ukitaka kupata kadi za visa zisizo unganishwa na account ya benki zenye uwezo wa kufanya malipo, itabidi kwenda kuulizia kwenye benki zilizo karibu na wewe kama wana option hiyo.

-(nyongeza)Kupata verified account ya paypal ndani ya nusu saa

Hii siyo lazima, kwa kuwa hatutokua tunatumia option ya paypal kwenye mafunzo ya PDF hii.

Paypal ni mtandao wa kutuma na kupokea malipo number moja duniani, unatumiwa na makampuni mengi sana makubwa, moja wapo ikiwemo ebay.

Kwa Tanzania paypal inatumika na watu baadhi, sanasana wanaonunua vitu na kulipia service mtandaoni. Haitumiku kupokea malipo kwa maana paypal bado hawajaja Tanzania kuweka makubaliano na bank mbili tatu ili kuweza kuturuhusu kupokea hela kutoka kwa mtu yoyote duniani.

Nataka tufanye juhudi za kupata account za paypal wengi Tanzania, kwa maana wakiona kuwa tupo wengi basi na wao watafanya juhudi kuturuhusu kuweza kupokea hela kirahisi kutoka nchi yoyote, na kwenda kutoa kutoka account zetu za bank.


So kwanza ili kupata account ya paypal inabidi uwe na kadi yenye visa au mastercard, ambayo inaruhusiwa kufanya manunuzi kupitia hizo njia. Ambayo tumeiongelea hapo juu.

Kuunganisha account yako na paypal ndani ya dakika 30


Hapa ni kwa wale wanaotumia account za UBA tu ambazo tumeziongelea hapo juu. Kwa wengine itachukua mda mwingi zaidi ya siku 3-5. Ukishapata kadi yako ya visa/mastercard. Hakikisha ina hela kidogo ndani yake angalau 10,000 Tsh.

-Hakikisha unapofungua account ya UBA unaunganisha na number yako ya simu ambayo ipo active wakati unajaza fomu.

-Utaingia paypal.com na kutengeneza account yako.




Chagua personal account



Kisha jaza information zako utazoulizwa.

Ukimaliza kujaza, una login kwenye account yako na kuweka information za kadi yako ya benki.



Utaambiwa uweke information za kadi yako zijaze kama zilivyo

Link a card

Card type

Card number

Expiration MM/YY


Save

Utapokea message kutoka UBA kuwa kuna hela imekatwa na paypal papo hapo. Takribani tsh elfu 7, na kutakua kuna code kwenye hiyo message ambayo ndiyo itakua yak u confirm account yako, code itakua kwenye mfumo huu PP*1234CODE , ukishajaza hii confirmation code basi utakua una uwezo wa kutumia account ya paypal kwenye tovuti yoyote inayokubali malipo haya.

CHAPTER 2: Kutafuta bidhaa (pamoja na tovuti ambayo tutakua tunaitumia sana)

Alibaba.com ni website kubwa kuliko zote duniani inayoruhusu mtu yoyote kuagiza bidhaa kutoka nchi za bara la Asia, sanasana china, Kwa bei nafuu kuliko sehemu au tovuti yoyote nyingine duniani. Kupitia alibaba unaweza ukaagiza nguo, penseli, mabati ya nyumba hadi mbegu za miti, chochote kinachoweza kuuzwa na kuagizwa utakikuta ndani ya alibaba. Alibaba.com inashughulika sana na watu wanao weka order za mizigo mikubwa hadi ma container na kuendelea, kuna njia nyingi za kupata bidhaa chache kupitia alibaba, ila kwa course hii hapa hatuto ingia kwenye topic ya alibaba.

Kwa kuwa hii ni kozi ya kuanza (bigginer) hatutokua tunaagiza bidhaa nyingi sana, yaani hatutokua tunaagiza ma container na ma container kwenye course hii, hatuto focus kwenye website ya Alibaba.com (tutaongelea alibaba kwenye advanced course baada ya hii), tunatafuta kuanza biashara polepole, biashara ambazo hata kama una mtaji wa shilling elfu 20, unaweza kuingia kwa kuagiza hata bidhaa moja tu, tutakua tuna focus kwenye aliexpress.com. Hapa ndipo nilipo anzia.



Aliexpress.com ni mtoto wa alibaba.com, humu ndipo ambapo mtu yoyote anaweza kuagiza bidhaa chache kutokana na uwezo wake, humu ndipo ambapo nilianza kwa kuagiza bidhaa mbili tu na kufikisha kuagiza mabox ya mamia na kuendelea kupitia aliexpress pekee.

So cha kufanya kwanza kabla ya kuendelea na kitu chochote kingine, ni kwenda na kufungua account <http://aliexpress.com>. Na kuanza kutafuta bidhaa ambazo utaweza kujikita nayo kwenye biashara utayoianza.

So step ya kwanza kwenye course yetu ni hii hapa

(YA MUHIMU : TAFUTA IDEA ZA BIDHAA ZAKO TATU HADI TANO UTAZOWEZA KUANZA NAZO)

Ukiingia aliexpress.com unaweza uka search kitu chochote. So shinda humu ndani, zunguka kila category angalia bidhaa zinazouzwa sana na ambazo zinapendwa, angalia bidhaa zitazokuvutia wewe na kama zinaweza kuvutia watu wengine pia. Natumiaga mda mrefu sana kuzunguka kwenye website kama hizi ili kutafuta bidhaa inayoweza kuja kuuzwa, fanya hivyo pia. Uwe na peni na karatasi pembeni ili uweze list down hizo bidhaa na kuzifanyia utafiti zaidi, bidhaa ziwe kuanzia tatu hadi tano.

Kwa bidhaa ambayo tunaitaka kuitafuta ni yenye sifa zifuatazo

-Bidhaa itayo rahisisha maisha ya mtu

-Bidhaa ambayo tutaweza pata faida kuanzia mara mbili hadi tano

-Bidhaa ndogo tu ambayo utaweza safirisha kirahisi na kupokea mzigo

-Bidhaa ambayo bado mpya na watu wengi hawaja anza kuuza hiyo bidhaa (competition ndogo)

-Bidhaa ambayo tiyari unaona zinauzika sana nchi zingine na huku bado hazija samba sana.

So ukiweza tick sifa mbili haditatu tu kati ya hizo tano za juu ujue bidhaa yako lazima itauza.

Tunazielezea hizi njia zote kwa urefu kwenye [advanced course](#)

CHAPTER 3: Kutengeneza brand

Ukitaka kukuza biashara yako ya mtandao kwa nyumbani inahitaji a lot of preparation and planning utaona watu wengi sana wanaagiza vizuri wanabahatisha vitu viwili vitatu kisha biashara inafeli, hii ni kuwa hawaja ji establish kama brand na wana deal kama individuals bado.

ukitaka uwe na biashara ambayo itakua kila siku na kuzidi ku tengeneza hela hata usipo ifanyia kazi yoyote kutangaza wala kupost kitu chochote basi ni muhimu ku brand vizuri biashra yako.

So tutachukulia mfano brand yangu ambayo niliitolea mfano kwenye post ya [NILIVYOWEKEZA LAKI MOJA HADI KUANZA KUTENGENEZA MILIONI MOJA](#)

1) Kutengeneza brand

Hamna step muhimu sana kama hii hapa, kutengeneza brand mapema kabla hata hujaanza kuuza kitu chochote, kuwa na logo ambayo mtu ataweza kukumbuka akitaka kurudi kununua bidhaa yako, au bidhaa nyingine ndani ya brand yako. Brand ina aminisha wateja kuwa kweli upo serious na unchokifanya siyo tu kama mamia ya wafanya biashara wadogodogo wanao weza kuuza vitu kwenye mtandao, njia pekee ya kuwa tofauti na kuaminika na kupata wateja wengi zaidi ni kuwa na brand.

Mimi nipo na business partner wangu, ambae tunafanya wote hizi kazi za kuagiza na kuuza bidhaa, tukishapata bidhaa tunayotaka kuiagiza na kuuza, tukiwa na uhakika kuwa tunataka kuwekeza mda kuuza hiyo bidhaa basi tunakaa siku nzima tukitafuta brand name, jina zuri ambalo litasimamia hiyo bidhaa au biashara. Sometimes inachukua hadi siku mbili au tatu kuweza kupata jina zuri la kutumia.

-Jinsi ya kutafuta jina (jina litaloaminika na wateja)

i) Cha kwanza ni kuangalia, brand kubwa wanajiita vipi na kupata ideas kutoka kwao.

- Watu ambao wanauza bidhaa kama zako, au bidhaa kwenye industry moja na wewe wanajiitaje, siyo hapo ulipo tu bali angalia dunia nzima watu wanaouza bidhaa kama yako wanajiitaje.

Kwa mfano, nikiwa nataka kuuza bidhaa za jikoni (kitchen supplies). Nitaingia facebook kwanza cheki link hii hapa <https://web.facebook.com/search/pages/?q=kitchen%20supply%20in%20tanzania>

Na pia ntaingia zoom Tanzania <http://www.zoomtanzania.com/biz/bed-bath-kitchen-stores/dar-es-salaam>

(Nagundua sahivi kuwa kuna brand chache sana za mtandaoni zinazo uza kitchen supplies baada ya kusearch hapo, so mtu anaweza kufikiria kujaribu sector hii la sivyo ntaingia mwenyewe)

Pia ninge google “kitchen supply stores” na kuona duniani watu wanauza kitchen supplies wakubwa wanajiitaje

Jina ni 30% ya mafanikio ya biashara yako, unapowaza jina waz amtu ataepiga simu na kuulizia brand yako, kwa mfano “hello, nyie ndio tiktok?”, hii tunapokea kila pale mtu atapo piga simu na kuulizia kitu

kutoka biashara ya tiktok Tanzania. Pia jina inabidi liwe rahisi ili mtu aweze kukumbuka kirahisi pale anapotaka kurudi kununua tena kitu kingine kutoka kwako.

(YA MUHIMU : TENGENEZA BRAND NA SOCIAL MEDIA ZAKE ZOTE SASA HIVI NA UZIKUZE)

-Tunatafuta jina ambalo lita represent ile bidhaa moja ambayo tunataka kununua, lakini at the same time jina ambalo linaweza simamia bidhaa nyingine ndani ya industry hiyohiyo, yaani kwa mfano mimi nauza saa za ukutani kupitia tiktokt, ila saa hizi zinge feli ningeweza endeleza hii brand na kuuza bidhaa nyingine inayo deal na interior designs, kwa kuwa hizi saa ni soko la interior designs.

So mfano pia mtu ameingia kwenye kitchen supplies ili kuuza bidhaa moja na akajiita mfano, “Jikoni Specials” hiyo bidhaa mda wake ukipita au soko likijaa sana, au watu wakaichoka tu hiyo bidhaa, anaweza aka agiza bidhaa nyingine inayohusiana na kitchen supplies na kuendelea kuuza kupitia brand hiyohiyo moja.

Hii ni muhimu kwa kuwa tiyari utakua una wateja ambao wanaijua brand yako, so hata kama ukiagiza bidhaa nyingine mpya, watakuja kuchukua kwako kwa maana wameshakujua.


-Jinsi ya kutengeneza Logo

Nawapa njia rahisi ya kutengeneza logo pamoja na cover photo, tafuta program ya photoshop kama hauna uliza mtu yoyote mwenye laptop kama wanamjua mtu mwenye photoshop, tafuta njia ya kuipata photoshop kwenye computer yako. Kwenye maisha yako kwa ujumla ukijua photoshop hata kidogo tu (haina kazi kabisa), itarahisisha maisha yako mara mia kwenye kufanya biashara.


Kutengeneza logo tutaingia website inaitwa [freepik.com](https://www.freepik.com)

Freepik ni website wanaotoa graphics material za bure ambazo unaweza ukazitumia kwa ajili ya project yako. So ukishaingia freepik.com tuta search biashara yako inahusu nini then tutaandika logo kwa mbele. Kwenye somo hili tutafanya kama tunatengeneza logo brand “Fahari Kids” hii brand yetu tuliyoitunga inauza bidhaa ambazo zitatumika na watoto wachanga miaka 1-5 hivi.

So tukiingia freepik tuta search “kids logo”



Na kwenye results zitazokuja tutachagua moja wapo ili kuitumia kama logo yetu. Tunataka brand yetu ione kane professional as possible sio kama imetokea out of no where. So tutachagua hii ifuatayo. Logo yenye nyota flani hivi



So logo ambayo tumeichagua ni kutoka kwenye list hii hapa.



So tutachotaka kufanya ni kuikata hiyo logo kutoka hapo na kuondoa maneno ya kids na kweka maneno yetu ambayo ni jina la brand yetu “Fahari Kids”. Ninaongolea jinsi ya kutengeneza logo mwenyewe kwa undani kwenye [advanced course](#), pamoja na promotional material ambazo ni muhimu sana ili kuuza.

Kwa kutumia photoshop au software ya bure iitwayo gimp tutakuja kupata kitu kama hiki




Ambayo ndiyo logo tutayoitumia kwa ajili ya hii brand yetu ambayo tumeitunga kwa ajili ya kufundisha somo hili. Jinsi ya kutengeneza logo hiyo Kama nilivyobadili hapo itafanyika kwa video kwa maana siwezi elezea kila kitu kwa maneno hapa. Kwenye videos pia tutaelezea jinsi ya kutengeneza header photo na promotional material pia. Kwa ajili ya brand yetu hii ya “Fahari kids”.


Chapter 4: Vya kuzingatia kabla ya kuagiza bidhaa yoyote kutoka mtandaoni

Kuna kanuni baadhi za kufuata ukiwa unaagiza bidhaa kutoka kwenye website ya aliexpress, ama website yoyote ambayo inafanya mauzo kwenye mtandao. Kwa kutumia Aliexpress tuta chukulia mfano huu ufuatao, hii ni baby carrier, hili ni soko kubwa sana kwa mtu ambaye atakua anatafuta sehemu ya kuwekeza.

Kwa kupitia aliexpress hii bidhaa ni karibia 10 USD pamoja na shipping, karibia elfu 23,000. [Link hii hapa](#)



Ukicheki jumia.co.tz baby carrier hizi hizi zinazuzwa kwa elfu 65,000. Ukitembelea hata maduka ya watoto mengine mjini, bei za baby carrier zimesimama from 60,000 hadi 100,000, so hapa ni wewe tu kuwekeza na kujaribu soko.



Okay so kabla hujaagiza bidhaa yoyote kwenye aliexpress, hivi ndivyo vya kuangalia.

1) Cheki review kutoka watu ambao wameshanunua

-Hii ndio sababu moja wapo kuu naipenda na kuiamini sana Aliexpress, reviews za watu wengine, wanaotumia wengi wanaikubali kwaajili ya sababu hii pia.

-Mtu akishanunua kitu, anarudi kwenye aliexpress na kuweka feedback ya alichokutana nacho baada ya kupokea mzigo huo. Hii inaonekana chini ya bidhaa tu ukiingia unakuta reviews zimejaa kibao kutoka watu tofauti tofauti. Kama hupendi ku risk, anzia kuagiza bidhaa ambazo watu wengi wamesha nunua, na kuacha feedback za kutosha.

-Aliexpress imejijenga vizuri kwa ajili ya hii feature peke ake, watu wamezoea sana kununua bidhaa kisha kurudi na kuacha feedback kuliko website yoyote inayouza bidhaa, so kama ni bidhaa inayonunuliwa vya kutosha utakuta reviews nyingi sana.

Tunaona kwenye mfano wetu hapa chini jinsi watu wana review hii bidhaa ya baby carrier.

Product Details
Feedback (3305)
Shipping & Payment
Seller Guarantees
Report item

5 Stars 295
4 Stars 41
3 Stars 7
2 Stars 0
1 Star 5

Average Star Rating: 4.8 out of 5 (348 votes)

All Feedback (397) All Stars (397) With Pictures (31) With Personal Information(0) Additional Feedback (13)

View reviews from Tanzania Translate to English Sort by default 2/40

AliExpress Shopper RU
Color: Purple Size: OneSize Logistics: China Post Ordinary Small Packet Plus
Thank you seller! all sewn quality) for the price, all the beauty!
29 Sep 2016 06:52
Additional Feedback
Really helps)) for the money just a beauty))) we have 10 kg and quietly stand))
04 Dec 2016 06:26

AliExpress Shopper SK
Color: Deep Blue Size: OneSize Logistics: China Post Ordinary Small Packet Plus
Everything is ok, good quality for this price, no smell, fast shipping... Thank you
03 Sep 2016 00:39

AliExpress Shopper US
Color: Purple Size: OneSize Logistics: China Post Ordinary Small Packet Plus
Super sling the quality is excellent, everything is adjustable for any child. our 3 months until all the straps are tightened completely. I asked prodovtsa specify a lower price all done. Shipping 2 weeks. thank you very much.
03 Sep 2016 00:35

Hapa tunaona watu ambao wameshanunua hizi bidhaa, wapo walioacha feedback, watu 397 kwa sasa, na kati ya hao walioipa bidhaa nyota tano ni 297, hii ni alama nzuri sana kwa bidhaa zaidi ya asilimia 75 ya watu walionunua wameridhika na bidhaa asilimia 100, bila tatizo lolote. Hadi hapo hii bidhaa kwa mimi ni nzuri na quality nzuri, na kama bado hujaridhika basi kuna watu kibao walionunua hii bidhaa na kuweka picha zao kuwa wamepata na wanaitumia bila shida yoyote. Picha kama hizi zifuatazo.



Ukitaka kuziona picha walizoweka watu, ukiwa kwenye page ya bidhaa, chini kwenye tab ya feedback, unabonyeza tu “with pictures” kama snapshot ifuatayo (siyo kila bidhaa watu wataweka pichalakini, baadhi sana)

Product Details **Feedback (3305)** Shipping & Payment Seller Guarantees Report item

5 Stars 295
 4 Stars 41
 3 Stars 7
 2 Stars 0
 1 Star 5

Average Star Rating: **4.8 out of 5** (348 votes)


All Feedback (397) All Stars (397) **With Pictures (31)** With Personal Information(0) Additional Feedback (13)

☐ View reviews from Tanzania ☒ Translate to English Sort by default 1/40

2) Hakikisha kuna njia ya kupata hela yako kama mzigo ukipotea au haujafika ndani ya mda mtaokubaliana

-Kwenye aliexpress, kama mzigo wako hauja upata, au umeharibika, au mda ambao mmekubaliana utapata mzigo umepita, wanakurudishia hela yako. Haitokei mara nyingi sana ila ipo mara chache ambao inatokea, hii ni kama unatumia njia za kusafirisha ambazo za bure na kuna mizigo mingi sana kwenye hizo njia, so mara nyingi hua na avoid njia za kusafirisha za bure, ntaelezea hili jambo zaidi kwenye chapter inayokuja.

Bhh



Kila bidhaa ya aliexpress ina hii buyer protection chini yake.

Yaani unaponunua bidhaa, hela yako inakaa na aliexpress haiendi kwa muuzaji, pale utapopokea mzigo na kuhakikisha kuwa upo kama ulivyotegemea ndipo unaweza kuingia kwenye aliexpress na kukubali kuwa umepokea, ndipo wanaachia hela yako iende kwa mtu anaeuza hiyo bidhaa, so unalipa, wanatuma, unapokea bidhaa, unahakiki kuwa umepokea bidhaa, ndio muuzaji anapokea hela.

3) Hakikisha mtu unaenunua kwake kweli ni mwenye hiyo bidhaa (wengine ni watu wa kati)

-Kuna baadhi ya wauzaji ndani ya aliexpress, ukiagiza kitu na wenyewe wanaagiza hapohapo wanakisubiri then ndo wanakutumia na wewe, hii inasababisha ule mda mrefu wa kusubiri ambao wengi wanalalamika. Ukiangalia kwenye feedback tafuta comment kama mtu amesema "seller shipped on time" au "item was shipped on time". Wanunuaji wa aliexpress wengi wanaelewa hiki kitu ndio maana wana comment juu ya hili swala.

-Ukiwa kwenye section ya feedback angalia kama kuna watu wengi wanalalamika kwamba "muuzaji hatumi vitu kwa wakati" (seller doesn't ship on time), hii inaonesha kuwa huyu muuzaji ni mtu wa kati na sio mwenye hiyo bidhaa.

-Pia kabla hujanunua, unaweza kumtumia muuzaji message kumuuliza kama bidhaa unayotaka kununua ipo in stock na mda gani itachukua hadi kutuma. "is the item in stock? And how long will it take to ship"

4) **Angalia njia wanayotumia kutuma, usipende free shipping tu mda wote**


Mizigo mingi ya free shipping wanachagua shipping ya bei ya chini sana kuliko zote ambazo huwa zinachukua mda mrefu sana hadi miezi miwili na kuendelea, kwa kuwa hizi njia zina tumika kutuma mizigo mingi sana. Mimi nina avoid kabisa free shipping ambayo haijasema inatumia njia gani kutuma mzigo. Nitaongelea njia zote za shipping kwenye chapter ifuatayo.

5) **Bei inayoandikwa siyo bei ya kuuza**


Bidhaa huwa zinaongezwa bei mara nyingi sana ili siku za sikukuu au siku za offer flani waweze kupunguza na bado wapate faida, so kama unanunua bidhaa zaidi ya moja (hata moja sometimes) hata kama bei ni ndogo vipi, muulize supplier anaekuuzia kama anaweza kukupa punguzo.

Siyo mda wote hii inakua ni kweli, ila kama asilimia 80 ya bidhaa utapata punguzo kama ukimtumia message muuzaji (supplier).

Kabla sijanunua kitu chochote huwa nauliza kwanza ka bei waliyoweka ndiyo bei bora zaidi, Mfano wa hapa chini supplier nilimuuliza akaniambia kuwa simu nliyokua nataka kununua haina punguzo.



Mfano huu unaokuja hapa chini niliuliza kabla ya kununua bidhaa na nikapata punguzo kutoka hadi USD 1020 hadi kufiki USD 360



brahim Amoo
2016-08-05 01:30

Dear yes DHL price

Order number: [redacted]
Status: Finished
Order Total: 1020.53 USD
Shipping: UPS Expedited
Contact Name: [redacted]
Address: [redacted] Dar-es-salaam Dar-es-salaam TZ
More Detail

Me
2016-08-04 09:41

DHL price?

Me
2016-08-04 09:30

I think DHL will be much better

brahim Amoo
2016-08-04 07:12

by UPS Expedited or by DHL
It will take 7 days about
Thanks
Wait you Msg
Thanks

Me
2016-08-04 09:28

Does ups charge customs when the package I in the country?

brahim Amoo
2016-08-04 02:34

Dear
360 \$ that is the best price shipping by UPS Expedited
How about it
Wait you Msg
Thanks

Me
2016-08-04 00:03

Hello... What is the best price for thus order?

Kuna video pia nitaionyesha jinsi ya kufanya ili kupata punguzo la bei kwenye aliexpress.

- 6) Angalia njia za kulipia kama unazo, inategemea na wapi unapotaka kufanya malipo ya bidhaa, mitandao mingi ya mazuo inahitaji kadi ya visa au mastercard tu, ila mtandao kama ebay ni lazima uwe na account ya paypal. Also unaweza ukawa una kadi ya visa/mastercard ambayo haijaruhusiwa kufanya malipo (nenda kwenye tawi la benki yako uulize kama kadi yako ina uwezo wa kufanya malipo kama hujawahi kufanya), kwa aliexpress tunahitaji kadi ya bank ya visa au mastercard ambayo imewezeshwa kufanya malipo, nimeongelea jinsi ya kupata kadi za kufanya malipo, kadi gani nnazo ziamini pamoja na kuwa paypal verified nakutumia paypal ndani ya nusu saa kwenye chapter ya kwanza kabisa.

Chapter 6: Jinsi ya kutafuta muuzaji anaeaminika

Okay tunaingia kwenye aliexpress.com, by now inabidi uwe na account tiyari kwenye aliexpress.com, inabidi uwe na application ya aliexpress kwenye simu yako, na ujue jinsi yaku navigate site nzima bila tatizo. By now umeshapata bidhaa zako mbili tatu na unataka kuweka order.


Tunaanza kwa ku search bidhaa tunayotaka.

Uzuri wa aliexpress ni kuwa ni ngumu sana kuibiwa au kutapeliwa hela yako kwa kuwa malipo yote yanafanyika ndani ya system yao na hamna malipo yanayoenda mojakwa moja kwa muuzaji hadi wewe utapokubali kuwa umepokea bidhaa ndipo muuzaji anapokea hela yake. Kama bidhaa uliyopokea ina shida yoyote unaweza weka malalamiko aliexpress watayapitia then wanakurudishia hela yako.


So supplier 95% ambao wanauza kupitia aliexpress wanaaminika na watatuma bidhaa, hata kama mda mwingine itachukua mda mrefu zaidi, zingatia mambo ambayo tumeyataja kwenye chapter iliyopita then you will be fine, tunachotaka ku avoid ni mda mrefu wa kusubiri bidhaa, na kutokupata bidhaa ambayo ipo chini ya kiwango.

utachoweza kufanya ni kuangalia vifuatavyo kutoka kwa muuzaji ili kupata supplier anaeaminika ambae utafanya nae kazi mda mrefu pale biashara yako itapokua.

Kwa kutumia mfano wetu ule wa baby carrier ngoja tuhakikishe kuwa ule muuzaji ni mzuri na anaaminika hata tukija kuendelea kufanya biashara ikiwa inakua. Ukiwa kwenye bidhaa yako nenda kwenye kipengele cha sold by, kisha ingia kwenye visit store.



Ukiingia kwenye store yake utaona bidhaa zake nyingi, sisi tunachotaka ni kuingia kwenye kipengele cha feedback kama ifuatavyo.



Kwenye kipengele cha feedback tutakuta Kama hivi kwa kila muuzaji, haya ndo muhimu sana kuzingatia.

Store Home Products Sale Items Top Selling New Arrivals **Feedback** Contact Details

Home > Store Home > Feedback Score

Service Center

offline
Contact Now

Store Categories

- Hot Selling
- Baby Toys
 - Baby Rattles & Mobiles
 - Play Mats
- Sticker
 - 50PCS
 - 100PCS
 - 150PCS
 - 200PCS
 - 300PCS
 - 500PCS
 - Other

Seller Feedback [Learn more about our Feedback Rating System](#)

Seller Summary

Seller: **Bestore Baby Co.,Ltd.**

Positive Feedback (Past 6 months): **97.7%**

Feedback Score: **21,460**

AliExpress Seller Since: **04 Jun 2014**

Detailed seller ratings


Item as Described :	★★★★★ 4.6 (3459 ratings)	11.38% Higher than other sellers
Communication :	★★★★★ 4.6 (3459 ratings)	13.02% Higher than other sellers
Shipping Speed :	★★★★☆ 4.4 (3459 ratings)	11.39% Higher than other sellers

Feedback History

Feedback	1 Month	3 Months	6 Months	12 Months	Overall
Positive (4-5 Stars)	432	1,427	3,249	8,138	22,058
Neutral (3 Stars)	13	46	91	213	740
Negative (1-2 Stars)	10	34	76	169	585
Positive feedback rate	97.7%	97.7%	97.7%	98.0%	97.4%

So kwenye “seller summary” hapa ndo kuna vitu vya muhimu kuzingati, tukianza na

- i) **Seller:** Hili ni jina la muuzaji ama supplier
- ii) **Positive feedback (past 6 months) :** Hii ni muhimu sana, hii inaonesha ni asilimia ngapi ya watu ambao wametoa feedback nzuri kwenye bidhaa zote anazozuza muuzaji, inapigiwa mahesabu ndani ya miezi sita ili muuzaji akibadilisha tabia, haya mahesabu na yenyewe yanabadilika.
- iii) **Feedback score:** hapa sasa ndio aliexpress wanapo fanikiwa ni kuwa rate hawa wauzaji kwa point za hizi feedback score, (nyota 5 au 4 stars ni sawa na pointi 1, nyota 3 ni sawa na pointi 0, na nyota 2 au 1 ni sawa na pointi -1) so muuzaji akipata nyota mbili au moja anapunguziwa feedback score yake kwa kuondolewa pointi moja, wauzaji wa aliexpress watajirahidi kila wawezalo ili waweze kukufurahisha wewe mteja ili uwawekee nyota tano na feedback score yao ipande. Ifuatayo ni picha inayoonesha feedback score kubwa kwa muuzaji inakuaje.



So muuzaji kama wetu tunaemchunguza kwenye somo letu ana point 21,460 kwa sasa na kama unavyoona hiyo picha ya hapo juu, yupo kwenye level nzuri, inabidi uzingatie sana hizi alama wanazopewa.

Kwa uelewa wangu muuzaji wowote mwenye pointi elfu 20 na kuendelea ni muuzaji anaeamika, na utafanya nae kazi vizuri sana.

- iv) **Aliexpress seller since :** Hapa inaonesha muuzaji amekua akiuza kwa muda gani, wauzaji baadhi huwa wakipata point mbaya nyingi sana kwenye store zao za aliexpress huwa

wanafunga account zao na kufungua mpya, hii inaonesha kuto kuaminika, ila mda mwingine wauzaji huwa wanafungiwa na aliexpress kwa kupinga baadhi ya sheria za aliexpress kama : “kutokuuza bidhaa batili ambayo inatengenezwa na kampuni kubwakubwa (counterfeit products)”. So hao pia huenda na kufungua account zingine. Muuzaji ambaye utamuamini kwa asilimia 100 kuwa utapa mzigo salam ni ambae amekua akiuza kwa miaka miwili na kuendelea, chini ya hapo ni wewe tu kuangalia inshara zote zingine ambazo tumeziongelea kabla.

v) **Detailed seller rating :** Hapa sasa ndo inavunja ratings za muuzaji kwenye vipengele vitatu muhimu

-Item as described : hii ni kama bidhaa anazozuza ndo kama anavyovielezea


-Communication: Hii ni kama ukimuuliza maswali anajibu vizuri

-Shipping speed: Hii ni kama muuzaji anatuma mzigo kwa wakati (hii pia inaonesha kama muuzaji ndiye mwenye bidhaa au ni mtu wa kati)

So vipengele vyote hivi vitatu vikiwa juu ya nyota nne ujue muuzaji anaaminika na bidhaa haina tatizo.

Chapter 6: Shipping option zote na maelezo yake

Kwenye chapter hii tutatumia example ya Leather wallets, tuseme tunataka uza wallet za leather na tunatafuta muuzaji ataekua ana shipping option nzuri tuki search aliexpress leather wallet zitakuja results nyingi sana, nnacho penda kufanya kabla sijaanza kutafuta ni kupanga matokeo ya search hiyo na kuona matokea yakianza "leather wallet" zilizounuliwa sana. (cheki picha ifuatayo uone nnapo bonyeza nkiwa natafuta bidhaa, imezungushiwa na blue)




So kila result hapa itakua imekuja na shipping option yake ya tofauti zimeandikwa kwa chini yake, ngoja nizielezee as many as I can. (uki weka mouse juu ya bidhaa utaona imeandikwa shipping option yake kame picha ifuatayo)




Aliexpress standard shipping

-Aliexpress standard shipping ni nzuri utapata tracking number nzuri, ila hauna control na jinsi gani mzigo utatumwa, muuzaji hapa anapeleka mzigo kwenye processing center za aliexpress na aliexpress ndio wanaochagua njia gani watatuma mzigo wako ambao utakufikia kwa haraka kutokana na uelewa wao, if I have no option nyingine ndio huwa nawatumia hawa, lakini nikiwa nina option nyingi na ipo shipping ninayo itaka sito itumia hii.



Seller shipping method

Sipendi sana kununua kitu kutumia “sellers shipping method”, ila kama there is a good deal unachoweza kufanya ni umuulize atatumia kwa njia gani atayo tumia? au achana nayo tafuta seller mwingine. Seller shipping method ni kwamba muuzaji ataamua atume kwa njia gani baada ya kupokea order yako, mara nyingi muuzaji atachagua njia yenye bei ndogo kulioko zote ili kupata faida zaidi, so hii option haito kuwa nzuri hadi umuulize kwanza ata tuma kwa shipping option gani.



Mashirika ya posta

Kila nchi ina shirika lake la posta, ambayo yote kwa pamoja yanashirikiana kutumiana mizigo kutoka nchi moja na nyingine, so mizigo ikiwa inakuja posta haimaanishi inatumia shirika hilo moja, hapana, kila shirika lina sheria zake za kutuma mizigo, lina mida tofauti inayotuma mizigo. So nashangaa sana pale mtu anapo lalamika kuwa posta wanachelewa sana kutuma au kuleta mizigo, shirika lipi la posta unalolitumia inabidi ujue. Mashirika makubwa ya posta yanayotumika aliexpress kwa kuwa wauzaji wengi wapo China, ni hongkong post na Chinapost.


Cha muhimu kwenye kuagiza mizigo ni mizigo itumwe kwa njia ambazo unapata tracking number nzuri, kuna tracking number nzuri na tracking number mbaya.

i) China post

Okay kwenye china post pia imegawanywa mara mbili kuna

China post Registered air mail

China post air mail, ipo vizuri mizigo inafika salama na wanakupa tracking number nzuri. Chinapost air mail wana process mizigo mingi sana kwa wakati mmoja so tegemea mzigo wako uwe processed kuanzia siku 5-10 kabla hata ya kutumwa lakini baada tu ya kuwa processed mzigo ukitumwa unachukua siku 5-7 tu kufika so mizigo kwa china post air mail kawaida inachukua wiki mbili hadi tatu kufika.



Na China post ordinary small packet


-China post standard mail ni ku achana nayo kabisa kama unataka mzigo haraka, mzigo utachukua mda mrefu sanaaa, na inatoa tracking number mbaya, ambayo hautoweza kutrack vizuri wala kujua mzigo upo wapi mara nyingi. Ni cheap sana ila njiamoja wapo ambayo mizigo ina uwezo wa kupotea ni hii hapa.



ii) Hongkong post

Hongkong post na wenyewe ni kama chinapost sema hawana mizigo mingi sana kama chinapost air mail, wata process mzigo siku 3-5 tu, baada ya hapo mzigo unatumwa. Hapa ni wiki mbili hadi tatu mzigo kukufikia.


Hongkong post wana tracking number nzuri.



Mengine ni haya yafuatayo


iii) Singapore post

Singapore post ni postaya singapore, hii inatoa tracking number nzuri, mizigo haichukua mda mwingi kuwa processed, siku 1-4 tu.. baada ya hapo mizigo inatumwa, kitu cha kuzingatia kuhusu Singapore post ni kwamba mizigo haiji moja kwa moja Tanzania. Mizigo ya Singapore post inafikia Kenya kwanza, alafu kutoka Kenya ndio mizigo inakuja Tanzania. So hapo ndo delay inapokuja kuwepo mizigo kutoka Kenya kuja Tanzania, mda mwingine ni siku mbili, mda mwingine ni tano hadi wiki. So kwa ujumla post NL na yenyewe itachuku wiki mbili hadi tatu hadi mzigo wako ukufikie.



iv) Post NL

Tunafikia sasa kwenye shipping options ninazo zikubali, postNL inatumika na baadhi ya wauzaji wa aliexpress. Hii haichukua mda ku process mzigo, inatumwa kwa wakati na mizigo inakuja moja kwa moja Tanzania, muuzaji akituma mzigo kwa wakati shipping hii inachukua wiki moja hadi mbili.



v) Turkey post

Tangu nianze kutumia aliexpress nimekutana na wauzaji wawili tu wanaotumia Turkey post na kwa ujuzi wangu this is the fastest way kupokea mzigo posta, turkey post hawana mizigo mingi wanayo iprocess kabisa, the fastest I have ever received a package kutoka hawa jamaa ni 5 days. Yaani siku tatu mzigo ukafika dar-es-salaam siku mbili waka process posta pale kisha mimi nikaenda kuuchukua. Siku zina vary siku 5-10 tu na hapa.

(Hao wengine siku nnazotaja sija include mda wa mzigo kuwa processed posta ukifika ambao inachukua siku 2-5)

Kuna wengine kama Sweden Post na swiss post ambazo pia zinafanya kazi kama Singapore post ila hazipo common sana.

- Mfumo wa tracking number, nzuri vs mbaya

Kwenye mifumo ya tracking number kwa mizigo inayokuja posta, kuna tracking number aina mbili ambazo hazitopoteza mzigo wako kamwe na mzigo utawahi, hizi tutaziita **“tracking number nzuri”** na kuna tracking number za mzigo ambazo ni mbaya na usipende kuzitumia kama upo serious na mizigo yako, hizi mzigo kuupata au kupotea ni bahati nasibu na mizigo itachelewa sana kwa kuwa kuna mizigo mingi sana inatumia huu mfumo wa tracking ambao tutauita **“tracking number mbaya”**, ambapo mizigo mingi sana inachanganywa ukipewa hizi tracking number.

Tracking number nzuri zina gharama inayozidi kidogo tracking numbe mbaya lakini it is worth it, kutopotelewa mzigo nilipoteza mizigo mingi sana wakati naanza kwa kuwa sikujua tofauti ya hizi tracking number.

-Tracking number nzuri

Hizi huwa zinaanza na herufi mbili mwanzo, namba nane kati kati na herufi mbili mwisho. Mfano ni hizi hapa chini.

International Shipping Company	Tracking Number
PostNL	RS60186606NL

International Shipping Company	Tracking Number
China Post Registered Air Mail	R171559010CN

-Tracking number mbaya

Hizi hazina mpangilio kama wa tracking number hizo za juu ni tofauti tofauti.. au herudi zimekaa sehemu za ajabu. Mfano huu hapa chini

International Shipping Company	Tracking Number	Remarks
Seller's Shipping Method	44730587955	

International Shipping Company	Tracking Number	Remarks
Other	E2007622780TZ	

Tracking number ndizo zita either poteza au kukuwahishia mzigo wako kwa haraka so ni muhimu kuwa makini nazo.

vi) DHL Fedex na wengine wakubwa Wengine

Hizi shipping ndio the fastest way ya kupokea mzigo, hazifai kama una mtaji mdogo na ndo kwanza unaanza, kwa kuwa ni gharama kubwa sana and also kila mzigo haijalishi ni mdogo vipi lazima utaulipia kodi, kuna exception chache sana.zinachukua siku 3-5 mzigo kukufikia ukishatumwa.

Chapter 7 Jinsi ya kutrack mizigo yako vizuri

Tracking ni njia ya kujua mzigo wako umefikia wapi tangu unapo uagiza tu hadi unapokuja kuupokea, mara nyingi posta hawakuambii kuwa mzigo wako umefika au number ya simu inaweza ikakosewa kwenye mzigo, au ukaweka information za P.O.BOX na wakatuma notice kwenye box lako, so ni muhimu kuwa na trackingnumber ili ukiona mzigo umefika unaenda kuulizia mwenyewe Box lako lilipokua.

Kwa wale ambao hawana box, sanasana kwa dar-es-salaam hii, sio lazima kuweka P.o.box, kwenye iformation zako. ukiweka tu jina kamili (jina kama lilivyo kwenye kitambulisho kinachotambulika) na number ya simu, unaenda post office ya posta mpya pale mizigo yote inapofikia na kuwapa tracking number yako ili wakupatie mzigo. Kila njia ya tracking ina sehemu yake tofauti ya kufuatilia mzigo.

Ila ni vizuri kutumia application hizi ambazo zina track mizigo yote, yaani tracking number yoyote ambayo ni nzuri haijali wapi imetokea kuna application ambazo zina track na kukuonesha mzigo umefikia wapi.

Nimetumia application nyingi sana kwa ajili ya hii process, lakini nimeiona moja tu ndio the best na inafanya kazi bila tatizo. Inaitwa 17track.


Kama unatumia simu ya android unaweza kuwa unaangalia mizigo yako kila inapofikia [17track android](#)

Kwa simu ya apple [17 track iphone app](#)

Kwa computer ingia tu [17track.net](#) na utaweza track mizigo yako yote humu.

Ukishalipia mzigo wako, wa taprovide tracking number baada ya mda, hiyo tracking number

Picha zifuatazo zinaonesha snapshot kutoka kwenye simu nikiwa natumia 17track



Ukiwa una track mzigo vizuri na una tracking number nzuri, unakufikia mapema tu na mzigo hauto kuja kupotea kamwe.

Conclusion

Ahsante kwa kupitia hii PDF I hope kama haujawahi kuagiza au kununua chochote hii itaweza kukusaidia kukusogeza in the right direction, kama utafanya kwa ajili ya biashara au kuagiza for personal use.

Kutafuta bidhaa na kwenda kupokea packages zinazotoka nchi zingine ni kitu ninacho furahia sana na najua wengi wanao fanya wana furahia pia. So cha kwanza ni kupata products na ndicho nilichoelezea kupitia introduction hii ya “biashara kwa mtandao”.

Baada ya introduction naamini utakua unaweza kupata kadi yako mwenyewe na kuagiza bidhaa yoyote na kwenda kuipokea baada ya mda, kufanya research ya bidhaa inayofaa kuagiza na mengineyo mengi mengi tu. Unaweza ishia hapa kama imetosha, kama una swali unaweza uliza kupitia facebook na twitter.

Kwa ambao watakua serious kwenye kufanya this as a business na kupata faida kuna mambo mengi sana mengine ya kujifunza ambayo tutayapitia kwenye [Advanced course](#) kama yafuatayo

- Tovuti tutazo tumia kutafuta bidhaa na kulinganisha bei
- kutafuta bidhaa ambazo lazima zitauza
- Kujaribu soko kuona kama lipo
- Kupata wateja kabla ya kuagiza chochote
- Kutengeneza na kukuza brand
- Kwanini branding ni muhimu
- Kutafuta jina la brand, kutengeneza logo na header photo
- Kutengeneza social media accounts
- Kutengeneza promotional material
- Kutengeneza pricing material
- Kuzi master Alibaba na aliexpress vs website zingine (maelezo)
- Suppliers / wauzaji wanaoaminika kwenye alibaba
- Kuagiza sample kuona quality
- Kuagiza na kupokea mzigo
- Kodi / TRA
- jinsi ya kupangilia bei
- Jinsi ya kupost for maximum exposure
- Wapi pa kupost ili kuuza bidhaa
- Kutangaza Facebook / Instagram / Google
- Authority indicators (zitakazo aminisha wateja mikoani na nje ya nchi)
- Kutengeneza website yako mwenyewe kwa gharama nafuu sana
- Kutengeneza email zako mwenyewe

Na mengine mengi yana patikana kwenye [advanced course](#) ambayo itafanyika mwezi mzima na zaidi kwa video na maelezo zaidi [bonyeza hapa kuipata](#).

